**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI**
**(EWURA)**

**NAMBA YA MALALAMIKO: GA.71/472/LZ/2024/25**
**NAMBA YA LOIS: COMP-2024-00000275**

**KATI YA**

**SELESTIN NDIBALEMA RWIZA ...................................................... MLALAMIKAJI**

**NA**

**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA ........................................... MLALAMIKIWA**

---

**AMRI**

---

***(Imetolewa na Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA tarehe 7 Mwezi Januari 2025)***

**MALALAMIKO HAYA** yameletwa mbele ya Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kwa ajili ya kutoa uamuzi leo tarehe 7 mwezi Januari 2025, kwa madai kwamba Mlalamikiwa aidha aondoe miundombinu ya umeme iliyopita katikati ya shamba la Mlalamikaji au kama haitawezekana amlipe fidia ya miti 20 iliyokatwa wakati Mlalamikiwa akiweka sawa mazingira ya kusimika nguzo hizo. Mlalamikaji ni mwenyeji wa Kijiji cha Ibalaizibu, Kitongoji cha kilete, Kata ya Kalabugaine, Mkoa wa Kagera.

Baada ya kupokea malalamiko tarehe 18 Septemba 2024, Mamlaka (EWURA) ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni

za EWURA za Utatuzi wa Migogoro *(EWURA (Consumer Complaints Settlement Procedure), Rules 2020)*) Gazeti la Serikali Na. 428/2020.

Mnamo tarehe 25 Novemba 2024, Mlalamikiwa aliwasilishautetezi wake na kuieleza Mamlaka kwamba miradi ya umeme vijijini inafadhiliwa na Serikali kwa lengo la kusaidia maendeleo ya jamii. Hata hivyo, kabla ya ujenzi wa miradi hiyo uongozi wa Serikali za Mtaa wa eneo husika hushirikiana na Wataalamu wao ili kufanya tathmini kwa kupita maeneo ambayo laini ya umeme itajengwa. Mlalamikiwa anaendelea kueleza kwamba kuhusu suala la fidia haitawezekana kwani miradi hiyo ina lengo la kukuza uchumi na maendeleo kwa jamii.

Kikao cha usuluhishi kilifanyika tarehe 28 na 29 Novemba 2024 katika Hoteli ya ELCT Bukoba iliyopo katika Manispaa ya Bukoba. Mlalamikaji aliwakilishwa na Bi. Milka Rwiza ambaye ni mtoto wake. Wakati wa kikao cha usuluhishi iligundulika kwamba mradi unaolalamikiwa uko chini ya Wakala wa umeme vijijini (REA) na bado haujakabidhiwa kwa Mlalamikiwa. Hivyo, kutokana na maamuzi ya awali yaliyofanywa na Mamlaka, rejea shauri la Zebedayo Kabepele dhidi ya TANESCO Mkoa wa Geita ambapo iliamriwa kwamba Mlalamikiwa alishtakiwa kimakosa hivyo hawezi kuwajibika kwa madai ya Mlalamikaji kwa muktadha huu. Mlalamikaji alishauriwa kupeleka madai yake REA ili aweze kudai stahiki zake.

Tarehe 11 Desemba 2024, Mlalamikaji aliiandikia Mamlaka barua ya kuomba kuondoa malalamiko yake kutokana na ushauri aliopewa siku ya kikao. Hivyo basi, Mlalamikaji anaomba kuondoa shauri lake EWURA.

Katibu wa Bodi **ANATOA AMRI** kwamba malalamiko haya yaondolewe na kila upande utabeba gharama za uendeshaji wa malalamiko haya.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hapa Dodoma leo tarehe 7 mwezi wa Januari 2025.

...............................
**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**